


## Mada ya Nne

### 1.4 Wanyama na Ndege



#### Misamiati

Vikembe  
Malighafi  
Mahiri  
Mazingira  
Kitega  
Uchumi

Mwishoni mwa mada hii, unatarajiwa kuwa na uwezo wa kutambua na kutumia misamiati inayohusiana na wanyama, ndege pamoja na vipengele vya lugha katika mawasiliano.

Unatarajiwa kuwa na uwezo wa:

- kutambua majina ya wanyama na ndege wa nyumbani na porini.
- kueleza faida za wanyama na ndege.
- kutambua vikembe mbalimbali .
- kusoma na kujadili makala yanayohusu sifa za wanyama na ndege.
- kubaini matumizi ya vivumishi vimilikishi katika sentensi.
- kutambua upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya A-WA katika sentensi.
- kuandika insha ya mwongozo kwa kufasiri michoro kuhusu wanyama

## Wanyama na Ndege

### Wanyama wa nyumbani

1.



Mbuzi



Ng'ombe



Punda




Farasi



Kondoo



Paka



Mbwa



Sungura



Nguruwe



Ngamia

### 3. Faida za wanyama wa nyumbani.

Mnyama		Faida
a)	Mbuzi	Nyama, maziwa , ngozi, mbolea.
b)	Ng'ombe	Maziwa, nyama, mbolea, ngozi.
c)	Punda	Kubeba mizigo, usafiri, mbolea.
d)	Farasi	Kubeba mizigo, usafiri, mbolea, michezo mbalimbali.
e)	Kondoo	Nyama, maziwa, sufu, ngozi, mbolea.
f)	Paka	kushika panya.
g)	Mbwa	ulinzi na usalama.
h)	Sungura	nyama, mbolea.
i)	Nguruwe	nyama, mbolea.
j)	Ngamia	kubeba mizigo, usafiri, nyama, mbolea, ngozi.

## UFAHAMU

### Faida za wanyama wa nyumbani

Wanyama wa nyumbani ni wale ambao wanakubali kufugika na kuridhiana na mwanadamu katika mazingira ya kinyumbani, bila ya madhara mabaya.

Wanyama hawa wafugwao wana faida chungu nzima kwa mwanadamu; kuna ngamia, ng'ombe, mbuzi, mbwa paka, sungura na wengineo. Miongoni mwao wamo waliwao na wale wasioliwa, ingawaje wasioliwa pia wana umuhimu wao mwingi kwa mwanadamu; kama vile mbwa ni mlinzi madhubuti, farasi naye ni hodari kwa ubebaji wa mizigo na usafiri. Paka ni msasi wa panya pamoja na nyingi nyinginezo katika faida zao.

Ama wale waliwao tukianza na ng'ombe ana manufaa makubwa katika harakati za ulimaji. Pakosekanapo trakta basi yeye huingia kazi, huchangia sehemu kubwa ya uchumi na maendeleo katika kilimo na ufugaji. Na kama ilivyo kawaida kuwa nyama zao ni kitowe, huliwa na kuuzwa pamoja na kutupa maziwa. Ngozi kama za ngamia, ng'ombe na mbuzi huleta pesa nyingi, kwani ni mali ghafi ya vifaa vingi kama vile viatu, mabegi, mikanda, majaketi, kofia, foronya za viti na kadhalika.

Ufugaji wa wanyama wote wa nyumbani waliwao na wasioliwa ni kitega uchumi kikubwa ambacho huleta maendeleo ya kiuchumi kwa mfugaji binafsi na taifa kwa ujumla.

### Msamiati

Mazingira: mastakimu/makazi

Madhubuti: enye nguvu/imara

Mahiri: mwenye maarifa ya hali ya juu.

Malighafi: kitu kiundiwacho vitu tofauti tofauti.

Kitega uchumi: kitu kiingizacho fedha.

### Jitathmini

- (a) Unaelewa nini kuhusu wanyama wa nyumbani kulingana na ufahamu huu?
- (b) Taja wanyama watano wa nyumbani waliwao.
- (c) Taja wanyama watatu wa nyumbani wasioliwa.
- (d) Eleza faida tatu za ng'ombe.
- (e) Ni vitu gani ambavyo hutengenezwa kwa ngozi za wanyama?

**4. Sarufi:****Ngeli ya A-WA**

Hii ni ngeli ya majina ya viumbe wenye uhai kama vile watu, wanyama , ndege, wadudu na kadhalika

Wanyama wote wa nyumbani hupatikana katika ngeli ya “A-WA”.

Mifano:

- a) Ng’ombe ana kula nyasi.  
Ng’ombe wana kula nyasi
- b) Punda anampiga mtoto teke.  
Punda wanawapiga watoto mateke.
- c) Farasi huyu anakimbia.  
Farasi hawa wanakimbia.
- d) Kuku yule ametaga yai.  
Kuku wale wametaga mayai.
- e) Bata mzinga anapenda kupiga kelele.  
Bata mizinga wanapenda kupiga kelele.

**Jitathmini**

Tumia majina ya wanyama wafuatao kuunda sentensi.


- (i) Mbuzi ...
- (ii) Kondoo...
- (iii) Paka ...
- (iv) Mbwa ...
- (v) Ngamia ...
- (vi) Sungura ...

## Jitathmini


Andika majina ya wanyama hawa katika wingi.

	Umoja	Wingi
a)	Ng'ombe	
b)	Mbuzi	
c)	Kondoo	
d)	Paka	
e)	Nguruwe	
f)	Farasi	
g)	Ngamia	

### Wanyama wa porini



Simba



Ndovu



Nyati



Twiga



Chui




Chui milia



Punda milia



Ngiri



Nyani



Tumbili



Sokwe



Fisi


### Jitathmini

Eleza faida mbili za wanyama wa porini.

Andika majina ya wanyama hawa wa porini kwa wingi:

- (a) Nyati
- (b) Ngiri
- (c) Simba
- (d) Twiga
- (e) Fisi

### Ndege wa nyumbani



Kuku




Njiwa



Jogoo



Kanga



Bata



Kifaranga



Batamzinga



**Jitathmini**

1. (a) Kwa nini tunafuga kuku nyumbani?
- (b) Je, mbwa ana umuhimu gani nyumbani?

**Ambatanisha wanyama/ ndege wafuatao na milio yao.****A**

Mbuzi  
Kondoo  
Kuku  
Paka  
Mbwa  
Bata  
Ng`ombe

**Ndege wa porini****B**

Klaak - klaak  
Kwaak - kwaak  
Mee-mee  
Moo-moo  
Bwoo - bwow  
Baa-baa  
Miaw - miaw



Korongo



Mwewe



Bundi



Tai

**Vikembe:**

Hawa ni watoto wa wanyama. Vikembe ni pamoja na:

	Mnyama	Kikembe
1.	Ng'ombe	Ndama
2.	Nzige	Kimatu/maige/ tunutu/ matumatu/ funutu
3.	ndege	kinda
4.	Kipepeo/nondo	kiwavi
5.	Nzi	Buu
6.	Farasi	Kitekli
7.	Mamba	Kigwena
8.	Nyangumi	Kinyangunya
9.	Fisi	Kikuto/bakaya
10.	Ngamia	Nirigi/nirih
11.	Paka	Kinyaunyau/kipusi
12.	ndovu	Kidanga
13.	Mbweha	Nyamawa
14.	Nyani	Kigunge

15.	Kondoo	Kibebe
16.	Mbuzi	Kibui/kibuli/kimeme
17.	Farasi/Punda	Nyumbu
18.	Punda	Kiongwe/kihongwe
19.	Mbu	Kiluwiluwi
20.	Chura	Kiluwiluwi
21.	Kuku	Kifaranga
22.	Papa	Kinengwe
23.	Nyuki	Jana
24.	Simba	Shibili
25.	Sungura	Kitungule
26.	Samaki	Chengo/ kichengo
27.	Chui	Kisui /chongole
28.	Mbwa	Kilebu/ kidue
29.	Nyoka	Kinyemere
30.	Njiwa	Kipura

**Sarufi:**

**Vimilikishi**

Nomino (umoja)	Vimilikishi	Nomino (wingi)	vimilikishi
Mbwa	wangu	Mbwa	wangu
Bata	wako	Bata	wako
Ng'ombe	wenu	Ng'ombe	wenu
Mbuzi	wetu	Mbuzi	wetu
Simba	wao wake	Simba	wao wake

Mifano katika sentensi:

Umoja

1. Bata wangu ni mzuri.
2. Mbwa wetu ni mkali sana.

Wingi

1. Bata wangu ni wazuri.
2. Mbwa wetu ni wakali sana.

3. Ng'ombe wake ni mnono.
4. Mbuzi wako si mfupi.
5. Simba wao si mdogo.

3. Ng'ombe wake ni wanono .
4. Mbuzi wako si wafupi.
5. Simba wao si wadogo.

### Jitathmini

Andika sentensi hizi katika wingi.

1. Mbwa wangu anakula nyama.
2. Dada yangu anafuga kuku.
3. Nguruwe huyu ni mchafu
4. Twiga yule si mrefu.
5. Batamzinga huyu si mbaya.

### Insha:

Andika insha kuhusu umuhimu wa wanyama unaowaona katika picha ifuatayo.

